

Ushirikishwaji wa jumuiya, ushirikishwaji wa vijana, na kuajiri viliendelea kuwa vipaumbele vya Ofisi ya Polisi katika mwaka 2021. Kwa usaidizi wa mashirika ya kijamii, vikundi vya ujirani, na shule, maafisa wetu walihusika kwenye zaidi ya matukio 150 ya jumuiya katika kila kona ya Jiji la Lancaster.

64,696

Wito wa Huduma

18

Matukio ya Ushirikishwaji wa Vijana

10

Matukio ya Ujirani

7

Malalamiko yaliyopelekea Nidhamu

530

Vijana walioshiriki Ligi ya Polisi (PAL)

127

Matukio ya Elimu ya SDOL

9

Matukio ya Kuajiri

MAELEZO KUTOKA KWA MKUU BEY

Dhima ya Ofisi ya Polisi ya Jiji la Lancaster ni kuwa jeshi la polisi lenye mwitikio wa kweledi na kivumbuzi lenye linalodhamiria kutoa huduma bora na kulinda jumuiya yetu.

Ili kutimiza dhima yetu, tunatumia mkakati wa kuishirikisha jumuiya, kuan-daa sera zinazozingatia data unaosisitiza maadili yetu ya msingi ya Huduma, Uadilifu, Heshima, Ujasiri, Kujitolea na Wajibu. Tunajiwajibisha wenyewe; sisi kwa sisi na kwa jumuiya yetu. Kila mhusika wa Ofisi hii, awe ameajiriwa kama askari au kama raia, anapimwa kwa mchango wake katika dhima yetu kuu. Tumedhamiria kuwa idara ya polisi iliyo wazi, inayowajibika, inayofiki-ka na yenye mwitikio kwa masuala ya jamii.

Usalama wa umma unapatikana kutohana na ushirikiano wa kuheshimiana kati ya jumuiya na polisi. Lazima tushirikiane ili kuunda jumuiya zenye uwezo wa kuendeleva maisha ya kiraia. Tuna wajibu wa pamoja wa kute-keleza majukumu yetu husika. Ofisi ya Polisi ya Jiji la Lancaster itatumia kila zana iliyonayo kuwa na mahali penye usalama. Mafanikio yetu kama Jeshi la Polisi yanategemea na kutoa huduma bora na kuanzisha mazungumzo thabiti ya jamii. Hivi ni vipengele muhimu vya ushirikiano wetu wa usalama wa umma.

JOHN T. BEY

Mkuu wa Polisi

MAFANIKIO MUHIMU

- Alianzisha Ofisi ya Ushirikishwaji wa Jumuiya, yenye waajiriwa 16 ambaa ni askari na waajiriwa 2 wa kudumu ambaa ni raia.
- Alianzisha upya Kitengo cha Doria ya Baiskeli kulingana na maoni ya wanajumuuya.
- Alianzisha mchakato wa kutambuliwa kwa jeshi la polisi, utakaojenga msingi thabiti wa upigaji zaidi wa hatua.
- Alipitia na kuandika upya Mwongozo wetu wa Sera kwa usaidizi wa wataalamu kutoha nje.
- Aliajiri mshauri wa nje kufanya uchambuzi wa masuala ya ndani na michakato ya malalamiko ya raia.
- Alipitia upya mchakato wa kuajiri, ikiwemo kuanzisha mchakato wa kuhoji (OB) waombaji.
- Aliajiri Mfanyakazi wa pili wa Masuala ya Jamii ili kuitumikia vyema jamii yetu.
- Aliongeza wingi na ubora wa mipango ya ushirikishwaji wa jumuiya



WASILIANA NASI

IKITOKEA DHARURA – PIGA 911

Taarifa isiyo ya Dharura – (717) 664-1180

Ofisi ya Utawala – (717) 735-3300

Wasilisha dokezo mtandaoni

kupitia LancasterPolice.com

MITANDAO YA KIJAMII YA OFISI YA POLISI YA JIJI LA LANCASTER

[Facebook.com/LancCityPD](https://www.facebook.com/LancCityPD) • [Twitter.com/LancasterPolice](https://www.twitter.com/LancasterPolice) • LancasterPolice.com



**CITY OF
LANCASTER**